

102/3
KISWAHILI
Karatasi 3
Fasihi
Julai/Agosti 2014
Muda: Saa 2 ½

KAMUKUNJI DISTRICT KCSE EVALUATION TEST 2014

MAAGIZO

Jibu maswali manne pekee.
Swali la kwanza ni la lazima
Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe
Kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:
Riwaya, Hadithi fupi, Fasihi simulizi na Ushairi.
Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

SEHEMU A: TAMTHLIA

Timothy Arege: Mstahiki meya

Swali la lazima

1. Jina si kitu. Tumbo ndilo muhimu. Tumbo lako na jamaa zako.
Watoto wako.

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)

(b) Taja mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili (alama 2)

(c) Eleza sifa zozote nne za mzungumzaji (alama 8)

(d) Dondoo hili linadokeza maudhui fulani katika tamthlia. Yataje na
Utoe mifano mingine miwili inayothibitisha maudhui hayo
(alama 6)

SEHEMU YA B: RIWAYA

KIDAGAA KIMEMWOZEA: KEN WALIBORA

2. "Nini hii? What is this?" aliingia ukumbizoni na kuuliza kwa ukali.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Taja kinachorejelewa na ueleze yaliyokipata kuanzia mwanzo
hadi mwisho. (alama 8)

(c) Taja na ufafanue mbinu ya uandishi inayotumiwa katika dondoo hili (alama 2)

(d) Eleza sifa za mzungumzaji katika dondoo hili. (alama 6)

3. Fafanua maudhui yafuatayo kama yanavyojitokeza katika riwaya ya Kidagaa kimemwozea:

1) Usaliti (alama 10)

2) Nafasi ya mwanamke (alama 10)

SEHEMU C

HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

4. "Kula mwanangu, hapana baya litakalotokea hapa. Wacha itikadi Yako mbovu".

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Fafanua maudhui ya itikadi/ushirikina kama yanavyojitokeza Katika hadithi fupi ya Gilasi ya mwisho makaburini. (alama 16)

5. Eleza hali ya shaka ya mambo inavyojitokeza katika hadithi ya Shaka ya mambo – (Farouk Topan) (alama 20)

SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI

6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Ewe Mainga wa Ndumi

Siwe uloambia akina mama

Siku tulopiga foleni

Chakula cha msaada kupata

Turudishe vifaranga kwenye miji

Wageuke vijusi tena

Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita

Matusi ukitema

Chumvi na Sukari kuturushia kama Samadi?

Uhitaji wetu ukatutuma

Kuokota vihela uloturushia

Ukatununua, kura ukapata?

Sasa miaka mitano imetimia

Waja tulaghai tena

Mainga wa Ndumi huna lolote safari hii

Ubunge umekudondoka ukitazama

Wanyonge tumeamua

Kwingine kujaribu.

MASWALI

(a) Huu ni wimbo wa aina gani?

Kwa nini?

(alama 2)

(b) Andika mbinu za lugha zilizotumiwa katika utungo huu. (alama 6)

(c) Ni nani anayezungumza katika utungo huu?

(alama 2)

(d) Fafanua ujumbe wa utungo huu

(alama 4)

(e) Fafanua umuhimu wa nyimbo za aina hii

(alama 6)

SEHEMU E: USHAIRI

7.SOMA SHAIRI HILI KISHA UJIBU MASWALI YANAYOFUATA

DUNIA

Dunia kitu dhaifu,
Usione ufanifu,
Kumbuka na uvunjifu,
Tagaa bovu dunia,

si ya mtu kunyetea,
na furaha kila njia,
kama ndwele hukujia,
ndu yangu silewelewe.

Anasa usiandame,
Heri moyo fanya tume,
Hakuna mume wa dume,
Tagaa bovu dunia

kwa pupa kuzipapia,
uche na kuzikimbia,
na wala hatatokea,
ndu yangu silewelewe.

Wako wapi mashujaa,
Ziliwafika nazaa,
Dunia ina hadaa,
Tangaa bovu dunia,

wenye nguvu kila njia,
wakabaki kujutia,
yataka kuzingatia
ndu yangu silewelewe

Kam kam Mahuluki,
Walokuwa na maluki,
Muda wakitahamaki,
Tagaa bovu dunia,

viumbe vyake jalia,
bora za kujivunia,
iliwatupa dunia,
ndu yangu silewelewe.

Fikiri zao sharafu,
Penye unasi alifu,
Mwisho wayo madhaifu,
Tagaa bovu dunia,

walizo wakitumia,
wanenalo maridhia,
na majina kupotea,
ndu yangu silewelewe.

Walishushwa ghorofani,
Wakawachia wandani,
Wameshia kaburini,
Tagaa bovu dunia,

mapambo na mazulia,
na mali zilosalia,
udongo kawafukia,
ndu yangu silewelewe.

Natarudi kwa Manani,
Kwa baraka za amini,
Tukafuzu duniani,
Tagaa bovu dunia,

tutubu zetu hatia,
mola tatughofiria,
mema na ahera pia,
ndu yangu silewelewe.

Turudipo kwa Jalali,
Kila sada tutanali,
Tutapata na uvuli,
Tagaa bovu dunia,

tukayawacha mabaya,
na shari kutwepushiya,
ahera kujifichiya,
ndu yangu silewelewe.

MASWALI

(a) Taja mambo ambayo mshairi anataka yaepukwe. (alama 4)

(b) Mshairi anatumia mifano gani kuonya na kueleza ujumbe wake?
(alama 4)

(c) Ueleze uhuru wa mshairi, ulivyotumika kwa kutolea mifano miwili tofauti: (alama 4)

(d) Andika ubeti wa 6 katika lugha nathari. (alama 4)

(e) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika. (alama 4)

(i) Nazaa.....

.....

.....

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

(ii) Kam kam.....

.....

.....

(iii) Tatughofiria.....

.....

.....

(iv) Madhaifu

.....

.....